

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**WIZARA YA MAMBO YA NDANI**  
**JESHI LA POLISI TANZANIA**

Telegraphic Address “”  
E-mail: dsmzhabari@gmail.com  
Telephone No.0222117705  
Faksi No: 022-2121524.  
Facebook: dsmzhabari  
Twitter; dsmzhabari1



Ofisi ya:-  
Kamanda wa Polisi,  
Kanda maalum ya Polisi,  
S.L.P.9140,  
**DAR ES SALAAM**

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

**UCHUNGUZI DHIDI YA HOSPITALI YA AGA KHAN YA JIJINI DSM  
KUTOZA GHARAMA KUBWA ZA MATIBABU.**

Jeshi la Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam limepokea malalamiko kutoka kwa wananchi dhidi ya Hospitali ya *Aga Khan* ya Jijini Dar es Salaam kutoza gharama kubwa za matibabu kwa wagonjwa wa matatizo kifua (**Pneumonia**) ambayo hupelekea matatizo ya upumuaji.

Aidha wagonjwa wanaopatiwa matibabu katika Hospitali hiyo, pindi wanapofariki dunia kumekuwa na tabia ya kuzuia miili ya marehemu na kudai kiasi kikubwa cha fedha kinyume na maelekezo ya Serikali kupitia Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto.

Jeshi la Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam baada kupokea malalamiko hayo limefungua Jalada la uchunguzi lenye

kumbukumbu namba **DSMZ/CID/PE/34/2021** dhidi ya malalamiko hayo.

Uchunguzi huu utakapokamilika na kubaini tuhuma hizi hatua kali za kisheria zitachukuliwa na Jeshi la Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama na Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto dhidi ya Hospitali hiyo.

***Katika tukio lingine,*** Polisi Kanda Maalum Dar es salaam ilifanikiwa kuwaua majambazi na kukamata silaha moja aina ya **Shortgun yenye No.MO1562004** ikiwa na risasi mbili ndani ya kasha.

Awali tarehe 17/02/2021 zilipokelewa taarifa fiche kuwa kuna majambazi wamepanga kuvamia duka la wakala wa Benki na mitandao ya simu huko maeneo ya kimara Stop over kwa kutumia pikipiki mbili, ndipo Polisi kupitia kikosi maalum cha kupambana na uhalifu waliwafuatilia majambazi hao wakiwa njiani ghafla wakagundua kuwa wanafuatiliwa na askari mara wakaanza kurusha risasi hovyoy, Polisi walijibu mashambulizi na kufanikiwa kuwajeruhi majambazi wawili na wengine wawili kutokomea na pikipiki mbili kusikojulikana na baada ya upekuzi eneo la tukio ilipatikana silaha hiyo na maganda matano ya risasi ya silaha aina ya bastola waliokuwa wakiitumia kurushiana na askari. Majambazi hao ambao umri wao unakadiriwa kuwa kati ya miaka

30-40 walipelekwa Hospitali ya Mlonganzila na daktari aligundua kuwa wamefariki baada ya kuvuja damu nyingi.

**Katika tukio la tatu**, kupatikana kwa silaha aina ya Bastola ya **Mhe.Nape Nnauye (Mb)** wa Mtama iliyoibiwa tarehe 15/02/2021 majira ya saa kumi na moja alfajiri huko nyumbani kwa maeneo ya Kawe Beach.

Bastola hiyo aina ya **GLOCK 17** yenye **No. YX647** ikiwa na risasi 14 ndani ya kasha lake. Silaha hiyo imekamatwa tarehe 17,02,2021 mkoani Mbeya baada ya ushirikiano wa Jeshi la Polisi Kanda maalum Dsm na mkoa wa Mbeya. Mtuhumiwa mmoja anashikiliwa kwa tuhuma za wizi wa silaha hiyo.

**LAZARO B. MAMBOSASA - SACP**  
**KAMANDA WA POLISI,**  
**KANDA MAALUM,**  
**18/02/2021**